



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI



13, FEBRUARY, 2023

**TANGAZO LA KAZI YA UFUNDI UJENZI KWA AJILI YA
UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA AWAMU YA PILI
(LGA/164/2022/2023/BW/FAC/II)**

**TANGAZO LA MARUDIO
NYONGEZA YA MUDA WA KUWASILISHA ZABUNI**

Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli imepokea fedha kwa ajili ya kuendeleza Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya eneo la Kwehangala.

Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli inapenda kutangaza nafasi ya Fundi Mjenzi wa Ujenzi wa Majengo mawili kama ifuatavyo;

1. Jengo la Kufulia LGA/164/2022/2023/BW/FAC/II/01
2. Jengo la Wazazi LGA/164/2022/2023/BW/FAC/II/01

Sifa za Fundi Mjenzi

1. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri michoro ya aina yote ya ujenzi
2. Awe na elimu/ujuzi wa kazi za ujenzi kwa kiwango chochote. Kwa mwenye vyeti aambatanishe.
3. Awe na uzoefu wa kufanya kazi katika majengo ya serikali. Orodhesha angalau miradi mitatu (3) ya serikali uliyokamilisha na mawasiliano ya taasisi husika
4. Asiwe ameshindwa kukamilisha mradi wowote wa serikali ndani na nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli
5. Awe na akaunti ya Benki iliyo hai
6. Awe Mtanzania
7. Awe na mafundi wasaidizi wa fani husika na vibarua wasiopungua nane (8).
8. Awe na uwezo wa kuendesha kazi mpaka atakapostahili malipo
9. Awe na namba ya mlipa kodi (TIN) toka Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Masharti ya kazi za ufundi

1. Fundi mjenzi anatakiwa kufika ofisi ya Afisa Manunuzi wa Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli kwa ajili ya kuchukua ramani na kujaza na *Schedule of labour Form* ya kuombea kazi za ujenzi.
2. Fundi Mjenzi Atatakiwa kujaza bei za kazi zote kwa kila hatua na kuweka viambatisho vyote husika
3. Fundi Mjenzi lazima afike eneo la Ujenzi ili kujirishisha na kazi kabla ya kuweka bei katika form atakayopewa.
4. Hakuna malipo ya awali (advance payment)
5. Malipo yatafanyika baada ya kufanya tathmini (evaluation) na kutolewa hati ya malipo (Interim payment certificate) iliyoidhinishwa na mtaalamu wa Ujenzi toka Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli
6. Malipo yote ya Fundi Mjenzi yatakatwa asilimia tano (5%) kwa ajili ya uangalizi (retention money)
7. Fundi Mjenzi atapaswa kuandaa mpango kazi kulingana na kazi zilivyoanishwa katika form ya kuombea kazi
8. Malipo yatakayofanywa yatakatwa makato yote ya kisheria yaani;
 - a. Kodi ya zuio asilimia tano (5% withholding tax)
 - b. Ushuru wa huduma (0.3% service levy)
9. Kazi zote zitasimamiwa na timu ya usimamizi wa mradi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ambaye atakagua, kufanya tathmini na kuidhinisha malipo yote.
10. Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli haitalazimika kukubali maombi ya gharama ya chini ikiwa vigezo vingine havitafikiwa
11. Mwisho wa kupokea maombi ni saa 04:00 asubuhi ya February 20, 2023 (Jumatatu) na kufunguliwa siku hiyo hiyo.
12. Maombi yote yatumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, 02 Kitongoji cha Ugunga, 21783 Bumbuli. Lushoto, S. L. P. 111, Bumbuli.
13. Kwa maswali na mawasiliano yoyote tafadhali piga +255 653 192625

me
Magdalena Utouh

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BUMBULI